

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

Nini maana ya hatua ya maandalizi ya filamu? Ninaweza kuomba nini haswa?

Kabla ya filamu kutengenezwa inahitaji kupitia "awamu ya maandalizi". Awamu hii ni hatua ya kwanza ya kila utengenezaji wa filamu na inajumuisha kukuza / kufafanua wazo la filamu, kuandika mswada, kupata fedha, haki shiriki, n.k.
Shughuli za maendeleo ambazo zinaweza kufadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Filamu ya DW Akademie ni pamoja na: (hii haina maana gharama zingine stahiki hazitakubalika) Kufanya kazi kwenye mswaada wako wa filamu, utafiti (kusafiri), kuandaa onesho la trela, kushiriki katika mafunzo (ada zamafunzo), kutauta fedha kwa ajili ya uandaaji (kufanyia kazi maombi ya kupata ufadhili zaidi), kusafiri kwenye matamasha, utafataji wa maeneo au wahusika, n.k.
Gharama za maendeleo ambazo unaweza kuomba ni pamoja na:

- gharama za utafiti zinazohusiana na mradi huo
- ada ya mhariri wa mswada
- ada ya mwandishi
- gharama za kusafiri zinazohusiana na mradi huo
- maabara, mikutano, gharama za kushiriki katika masoko ya filamu
- gharama za uandaaji wa trela
- gharama nyinginezo (vifaa vinavyohusiana na mradi kama simu, kodi ya ofisi, n.k.)
- ada ya upatikanaji wa haki miliki
- ushauri wa kisheria

Ninaweza kuomba kiasi gani cha fedha?

Unaweza kuomba hadi euro 10.000 kulipia gharama zinazostahiki kwa awamu ya uandaaji ya mradi wako wa filamu.

Ni kiasi gani cha fedha inayoombwa inaweza kutumia katika nchi husika ya mwombaji?

Waombaji wanapaswa kulenga kutumia fedha nyingi iwezekanavyo katika nchi yao. Lakini, si lazima gharama zote za awamu ya maendeleo kutumika katika nchi ya mwombaji. Kwa hivyo, tafadhali onyesha mpangokazi wako, pamoja na ratiba na mahali ambapo shughuli zako zitafanyika.

Lugha gani inatumika katika kuwasilisha maombi?

Tunaomba maombi yawe kwa Kiingereza. Ikiwa maombi yatajumuisha nyaraka zilizo katika lugha tofauti, tafadhali ambatisha tafsiri yake ya Kiingereza.

Supported by the Federal Ministry for Economic Cooperation and Development

DW Akademie Film Development Fund



Je! Ni nyaraka zipi ninahitaji kuwasilishwa?

- Fomu ya maombi
- Mwongozo (hadithi za kubuni: zisipungue kurasa 20, hadithi za makala zisipungue kurasa 7)
- Ratiba ya shughuli: onyesha muda na mahali kwa kila shughuli iliyopangwa kufanyika kwa kipindi cha mwaka moja, sambamba na matokeo yanayotarajiwa.
- CV

Waombaji ambao miradi yao imechaguliwa wataulizwa kuwasilisha yafuatayo:

• toleo la hivi karibuni la mwongozo au mswada
• bajeti
• ikiwa inapatikana: uthibitisho wa kuwepo kwa hakimiliki.
DW Akademie itawasiliana na wewe ikiwa mradi wako utachaguliwa.

Mwongozo ni nini?

Mwongozo wa filamu huandikwa kabla ya kuandika mswada. Ni ufupisho wa hadithi ya filamu. Mwongozo huwa ni andiko fupi sana kuliko mswaada wa filamu na kawaida huwa haina mazungumzo ya kina. Inapaswa kusoma kama hadithi fupi, inayosimuliwa kwa wakati uliopo.
Tafadhali wasilisha kurasa ishirini (20) kwa mwongozo wa filamu za kuigiza na kurasa saba (7) kwa filamu za makala. Tafadhali andika mwongozo kwa lugha ya Kiingereza.

Ninaishi nje ya nchi yangu kwa kipindi fulani cha mwaka. Je, bado ninaweza kuomba?

Watengenezaji wa filamu kutoka ughaibuni kwa bahati mbaya hawaruhusiwi kuomba. Maombi yatakayokubalika ni kwa wale wanaoishi na kufanya kazi katika nchi inayopata ruzuku hii. Ikiwa wewe ni raia anayeishi nje ya nchi kwa zaidi ya miezi mitatu kwa mwaka, tafadhali wasiliana na DW Akademie kabla ya kuomba: dw-akademie.film-fund@dw.com.
Maombi ya aina hiyo yataangaliwa kulingana na mazingira au sababu iliyotolewa.

Kipindi cha ufadhili ni cha muda gani? Kinaanza lini?

Kipindi cha ufadhili ni cha mwaka mmoja na huanza siku ambayo ruzuku inatolewa rasmi au kutangazwa rasmi. Lakini malipo yataanza kutolewa baada tu ya makubaliano na mikataba yote kukamilika. Iwapo mwombaji ataanza kufanya malipo yeyote kabla ya kumalizika kwa taratibu za kisheria, na basi gharama hizo zinaweza zisikubalike kuwa sehemu ya ufadhili.

Kwa nini natakiwa kutoa maelezo ya mahitaji yangu ya mafunzo katika maombi yangu?

Ili tuweze kutoa mpango wa mafunzo mahsusi kwa mlengwa na kukidhi mahitaji yake, tunahitaji taarifa za kina juu ya maeneo ya uhitaji wa mafunzo yatakayomsaidia kutekeleza mradi vizuri na kuongeza taaluma.

Supported by the Federal Ministry for Economic Cooperation and Development

DW Akademie Film Development Fund



Je! Mafunzo yenyewe yatahusu nini hasa?

Kila mtengenezaji wa filamu aliyechaguliwa ataambatanishwa na mshauri mtaalam wa kimataifa ambaye atamwongoza kupitia mchakato wa uendelezaji wa mradi kwa mwaka mzima.
Kwa nyongeza, DW Akademie itatoa fursa zaidi za mafunzo yaliyoandaliwa maalum kwa kuzingatia viwango tofauti na nyanja mbalimbali za wale wote waliochaguliwa. Mafunzo yataandaliwa kulingana na mahitaji ya washiriki.

Je, kushauriana na DW Akademie ni lazima kabla ya kuomba?

Hapana. Kushauriana baina ya waombaji na DW Akademie sio lazima, lakini tunapendekeza sana ushiriki wako kwenye kikao cha Maswali na Majibu mtandaoni kitakachofanyika muda mfupi baada ya wito wa maombi kuzinduliwa. Mkutano utakupa taarifa juu ya utaratibu wa maombi na pia utaweza kuuliza maswali moja kwa moja kwa DW Akademie. Tarehe ya mkutano itatangazwa kwenye tovuti.

Ni nini uthibitisho wa uhodhi wa haki miliki?

Kwa uthibitisho wa haki miliki, mwombaji anahakikisha umiliki wa haki zinazohitajika ili kutekeleza mradi wake. Mwombaji athibitishe anayo haki miliki na kuwa anazo ruhusa zote zinazohitajika kutekeleza mradi huo.
Ikiwa filamu yako inajumuisha vitu ambavyo vinahusisha kikamilifu, au hata kwa kiwango kidogo, kazi nyingine yenye umiliki tofauti (kwa mfano filamu nyingine, kitabu, wimbo, n.k.) utahitaji idhini au haki zinazohitajika ili kutekeleza mradi wako. Kupata ruhusa hizi za kisheria ni sehemu muhimu ya mchakato wa uandaaji ya mradi.
Mfano:
• makala ya wasifu kuhusu mtu halisi; kwa hili utahitaji “haki za maisha” kutoka kwa mtu huyo au wasihi wake
• kugeuza kitabu kuwa filamu ya kuigiza; kwa hili utahitaji haki za kutohoa kutoka kwa mchapishaji.
• filamu fupi inayohusu lebo maalum ya rekodi; kwa hili utahitaji haki za muziki kwenye rekodi husika.
Unaweza pia kuhitaji kibali cha ziada kinachohusiana na video za kumbukumbu, nyimbo, mahali, picha na nukuu za fasihi.

Bado sina uthibitisho wa haki miliki. Je! Bado ninaweza kuomba?

Ndio, unaweza kuomba ikiwa bado hauna idhini au haki zinazohitajika za kutekeleza mradi wako. DW Akademie itawasiliana na wewe ikiwa mradi wako umeorodheshwa na bado haujasilisha uthibitisho wa hakimiliki.

Nitajuaje ikiwa umepokea maombi yangu?

Utatumiwa uthibitisho utakaokutaarifu kwamba tumepokea ombi lako na kwamba uwasilishaji wako umekamilika. Tafadhali usiwasiiane na ofisi yetu ili kudhibitisha maombi yako.

Je nitajulishwa kuwa mradi wangu umepita?

Ndio, tutawasiliana na wewe ikiwa mradi wako utakuwa umepita ama kuchaguliwa.



Nitajua lini ikiwa nimechaguliwa?

Tutakujulisha kwa barua pepe iwapo jopo la majaji litakuwa limepitisha mradi wako, na kukujulisha mara tu uamuzi utakapofanyika. Tafadhali kumbuka kuwa hii itakuwa takriban miezi miwili baada ya tarehe ya mwisho ya maombi kupita.